**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu:**

**Mkuu wa Shule: 0756510222/0656384329**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0629467808**

**Mhasibu wa Shule: 0757142467/0621006663**

**Shule ya Sekondari Matai,**
**S.L.P. 75,**
**Matai – Kalambo.**
**Juni, 2026.**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MATAI HALMASHAURI YA KALAMBO KATIKA MKOA WA RUKWA**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ………. na atasoma tahasusi ya ………….

Shule ya Sekondari Matai ipo umbali wa Kilometa 2 Kusini/Mashariki mwa Mji wa MATAI, Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi Sokomatola (STANDI YA ZAMANI SUMBAWANGA MJINI) Nauli ni Shilingi 4,000 kutoka Mjini Sumbawanga mpaka Matai, na ukifika matai pikipiki ni shiligi 2,000 kutoka matai center mpaka shuleni na Shilingi 2,000 kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza Juni, 2026 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe …………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …………….

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**2.1 Sare za Shule**

I. Sare ya shule hii ni suruali ya light-blue na Kaki.

.

**Maelezo ya mshono suruali**

(a). iwe pana chini na iwe na sellebration.
(b). Mashati 02 meupe mikono mirefu.

II. Sare ya Michezo ni trucksuti nyeusi jozi moja

na raba za michezo jozi moja rangi yeyote.

III. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
IV. Soksi jozi mbili nyeupe za shule na mkanda mweusi wa kuvalia suruali.

V. Nguo za kushindia trucksuti moja ya light blue na t-shirt ya light blue.

VI. Suruali moja nyeusi kwa ajili kushindia na kwendea kwenye ibada, isiwe jeans.
VII. Tai mbili ya lightblue na kaki zinazoendana na rangi za suruali.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari TISA COUNTER BOOK QR 3.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka.
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa mchepuo wa HGE.
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe la nchi mbili na nusu.
vi. Mashuka ya rangi ya lightblue Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1.
vii. Nguo za ndani za kutosha.
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko.
x. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa (ndani 01 na nje 01) & mopa 01.
xi. Sweta moja la shule na T-shirt Mbili za shule (Kola na Round) vinavyopatikana shuleni kwa gharama ya sh. **45,000/=.**

**NB**: **Mwanafunzi aje na hela kwa ajili ya ulipaji na upatikanaji wa T Shirt hizo na sweta ni lazima kuwa navyo vitu hivyo kwani ni sare ya shule**.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB**:

I. **MCHANGO WA UENDESHAJI UWEKWE KWENYE AKAUNTI NAMBA 62101100050 JINA MATAI SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTION.**

II. **MCHANGO MINGINE IWEKWE KWENYE AKAUNTI NAMBA 62101100048 JINA MATAI SECONDARY SCHOOL SELF RELIANCE.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

### 3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

x. Kusababisha mimba;
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**Karibu sana katika shule hii**

**…………………....**

**PIUS I. KWIMBA**
**Mkuu wa Shule.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0756510222/ 0656384329**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0629467808**
- **Mhasibu wa Shule: 0757142467/ 0621006663**
- **Mwandamizi Taaluma: 0769296469/ 0621638316**